WORLDCOIN FOMU YA IDHINI YA DATA

**Idhini ya Kusindika Data Nyeti na Idhini ya Kutuma Data Nje ya Nchi Yako**

**Muhtasari Mfupi wa Idhini hii ya Data.**

Muhtasari huu unakusudiwa kukusaidia kuelewa kwa haraka kile ambacho unaombwa kukubali. Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, maelezo ya ziada yametolewa chini ya muhtasari huu.

Ukikubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data, unaruhusu Worldcoin **kukusanya** data zifuatazo:

- Picha za kina za viini vya macho yako;
- Picha za kina za uso wako (kichwa na mabega); na
- Ramani halisia za uso wako (kichwa na mabega).

Pia unaruhusu Worldcoin **kutuma** data hii kwa timu zetu zilizo katika Umoja wa Ulaya (kwa sasa nchini Ujerumani na Polandi), India, Uingereza, na Marekani kwa malengo tu ya kufunza teknolojia yetu, kama ilivyobainishwa hapa chini.

**Si lazima uidhinishe ukusanyaji na utumaji wa data hizi ili uweze kushiriki katika Worldcoin.** Bado unaweza kuunda akaunti na kuwa na pochi la Worldcoin bila kukubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data, ingawa bado utahitajika kukubaliana na Kauli ya Faragha ya Worldcoin (getworldcoin.com/Privacy). Ukichagua kutokubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data, hautaweza kushiriki katika vipengele fulani vya Worldcoin, kama vile kupokea kiwango kidogo cha WLD bila malipo au kuwa na utambulisho wa kipekee wa kidijitali.

**Unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote kwa kutumia lango letu la maombi linalopatikana kwenye anwani: http://worldcoin.org/requestportal .**

Matumizi na usindikaji wa data zako na Worldcoin unatawaliwa na hati mbili: Kauli ya Faragha ya Worldcoin (getworldcoin.com/Privacy) na Fomu hii ya Idhini ya Data. Kauli ya Faragha inasimamia data zinazokusanywa na kusindikwa kupitia tovuti, programu, na huduma nyingine za Worldcoin, nayo Fomu hii ya Idhini ya Data inaelezea jinsi tunavyokusanya, kutumia, kuhifadhi na kufuta data zako za bayometriki zilizokusanywa kupitia Orb yetu. Hati hizi zinaendanisha moja kwa moja, na zote mbili ni muhimu katika kuelewa faragha ya data zako katika Mradi wa Worldcoin. Fomu hii ya Idhini ya Data imejumuishwa kwenye na inatawaliwa na Sheria na Masharti ya Mtumiaji wa Worldcoin (getworldcoin.com/terms).

1. **Mradi wa Worldcoin.**

Worldcoin inataka kujumuisha watu wengi zaidi kadri iwezekanavyo katika Intaneti mpya bila mtawala mkuu, ambayo wakati mwingine inaitwa “web3.” Ili kufanya hili kwa haraka, Worldcoin itamruhusu kila mtu kuchukua mgao wake wa sarafu ya kidijitali ya Worldcoin (WLD) bila malipo. Ili mradi huu mkubwa kufaulu, ni lazima Worldcoin ihakikishe kwamba kila mtu anayejisajili ni binadamu aliye hai (si roboti au mnyama, kwa mfano) na kwamba wanajisajili mara moja pekee. Aidha, Worldcoin ni lazima ifanye hili kwa njia ambayo inalinda faragha na usalama wa data wa kila mtumiaji. Unaweza kusoma mengi zaidi kuhusu mradi wa Worldcoin kwenye tovuti yetu.

2. **Orb.**

Orb ni kifaa cha kibinafsi kinachosuluhisha tatizo lililoelezewa hapa juu. Inathibitisha wewe ni “binadamu wa kipekee” huku ilihakikisha faragha yako. Orb inapiga picha kadhaa za ubora wa juu zaidi za macho yako (haswa, viini vya macho yako) na uso wako (kichwa chako na mabega yako). Baadhi ya picha hizo zinatumika kuthibitisha wewe ni binadamu halisi, aliye hai. Picha za viini vya macho zinageuzwa na kuwa **kitambulishi cha kipekee** – huu ni msururu wa nambari ambao unatumiwa kubaini kana kwamba ulikuwa umejisajili tena hapo awali kwenye kifaa cha Orb. Kitambulishi hiki cha kipekee kinatengenezwa kupitia utendaji wa “one-way hash” ambao unaondoa kabisa uhusiano baina ya picha hizo na kitambulishi cha kipekee, na kudumisha faragha.

3. **Majaribio Nyanjani.**

Worldcoin bado inajitahidi kuboresha utendakazi wa Orb na kuimarisha mfumo unaobaini kama mtu anastahiki kupokea mgao wa Worldcoin bila malipo. Awamu hii ya utengenezaji tunaita majaribio nyanjani.

Tungependa usaidizi wako katika awamu hii ya majaribio nyanjani. Haswa, bado tunaimarisha teknolojia ya programu ambayo inatumia picha za uso na macho yako ili kutengeneza kitambulishi cha kipekee. Ili kuboresha usahihi wa teknolojia hii, tunahitaji kufunza teknolojia hii kwa kutumia picha kutoka kwa watu halisia kama wewe.

Hii inamaanisha kwamba tunakuomba idhini yako ya kutuma picha hizi za uso na macho yako kwa timu za Utafiti na Utengenezaji kwa malengo yaliyoelezewa hapa chini. Ushiriki wako ni wa muhimu sana katika kusaidia Worldcoin kukamilisha majaribio nyanjani na kufanikisha misheni yake. Ushiriki wako si wa lazima, lakini tutashukuru sana.

4. **Usahihi.**

Kulingana na hali na mafunzo ya teknolojia (machine learning), huenda teknolojia ikasema kwamba tayari umechuku mgao wako wa Worldcoin. Kwa wakati huu, Worldcoin haina mfumo wa watumiaji kuripoti hitilafu zilizoko au kupinga uamuzi wa teknolojia. Ukikubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data, unatupatia idhini yako ya uamuzi huu otomatiki kama ilivyoelezewa hapa juu.

5. **Idhini Si Lazima ili Kushiriki katika Worldcoin.**

Si lazima ukubaliane na Fomu hii ya Idhini ya Data ili kushiriki katika Worldcoin. Bado unaweza kuunda akaunti na kuwa na pochi la Worldcoin bila kupatiana idhini hii, ingawa bado utahitajika kukubaliana na Sheria na Masharti ya Mtumiaji wa Worldcoin (getworldcoin.com/terms) na Kauli ya Faragha ya Worldcoin (getworldcoin.com/Privacy). Aidha, ukichagua kutokubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data, basi hautaweza kushiriki katika vipengele fulani vya Worldcoin, kama vile kupokea kiwango kidogo cha WLD bila malipo au kuwa na utambulisho wa kipekee wa kidijitali.

6. **Data Tunazokusanya.**

Kwa idhini yako, tunakusanya data zifuatazo kwa kutumia Orb:

- **Picha za kina za viini vya macho yako.** Picha hizi zinapigwa kwa kutumia teknolojia ya “visible”, “near-infrared” na “far-infrared”. Zinatumika kutengeneza kitambulishi cha kipekee na, wakati wa awamu ya majaribio nyanjani, kufunza teknolojia jinsi ya kupiga picha bora na kutengeneza vitambulishi vya kipekee bora. Kama ilivyotajwa katika Sehemu ya 4 hapa juu, teknolojia hii si timilifu na huenda ikafanya makosa, kama vile kubaini kimakosa kwamba tayari umepata mgao wako wa WLD bila malipo. Tunatumia picha hizi za kina za viini vya macho ili kufunza teknolojia hii na kuboresha utendakazi wake, ili hitilafu kama hizo zipungue kabisa.
- **Picha za kina za uso, kichwa na mabega yako.** Picha hizi zinapigwa kwa kutumia teknolojia ya “visible”, “near-infrared”, na “far-infrared”. Zinatumiwa kugundua ulaghai na, katika awamu ya majaribio nyanjani, kufunza teknolojia yetu kutambua macho yako kwenye uso wako jumla.
- **Ramani halisia za uso, kichwa na mabega.** Picha hizi zinatumiwa kutusaidia kugundua ulaghai.

**Muhimu**: Katika kuchukua picha hii ya kiini cha jicho, tunatumia sifa zako za kimwili, kimienendo, au kitabia (yaani, mtindo wa kiini cha jicho lako) ili kukutambua kama binadamu wa kipekee. Katika baadhi ya nachi, data za aina hii zinazingatiwa kuwa bayometriki na huenda zikawa chini ua ulinzi za ziada.

7. **Tunachofanya na Data Hizi.**

Kwa idhini yako, tunatumia data zilizo hapa juu kwa malengo yafuatayo **pekee**:

- Kutathmini vitambulishi vya kipekee;
- Kulinganisha vitambulishi vya kipekee;
- Kuimarisha tathmini za vitambulishi vya kipekee;

- Kutengeneza na kufunza teknolojia ya kutambua na kutofautisha viini vya macho vya binadamu tofauti;
- Kuondoa hitilafu kwenye teknolojia yetu ya kutambua viini vya macho;
- Kutengeneza na kufunza mfumo wa kugundua kama mtumiaji ni binadamu au la;
- Kutengeneza na kufunza miigo inayotumia picha za viini vya macho vya kutengenezwa kwa ajili ya mafunzo zaidi ya teknolojia; na
- Kufunza na kukutathmini wafanyakazi wanafanya kazi kwa kutumia mifumo hii.

8. **Utumaji Data.**

Wakati Worldcoin inapotumia data zako kwa malengo yaliyo hapa juu, kwa ujumla tunatuma data nje ya nchi ambako inakusanywa na kutumwa kwa timu zetu za Utafiti na Utengenezaji. Timu hizi kwa sasa ziko katika Umoja wa Ulaya (kwa sasa nchini Ujerumani na Polandi), India, Uingereza, na Marekani.

Tunaambatana na misimamo iliyotajwa katika Kanuni Jumla ya Ulinzi wa Data (General Data Protection Regulation, “GDPR”) za EU, kama sera. Kwa mfano, hata ikiwa nchi yako na sheria za faragha ya data ambazo ulinzi wake ni mchache kuliko GDPR, bado tunasindika data zako kulingana na GDPR. Pia tutatumia tu data zako kwa malengo yaliyotajwa hapa juu, hata ikiwa sheria za faragha ya data nchini mwako hazingezuia jinsi tunavyotumia data zako.

9. **Hatari Zinazoweza Kukumba Utumaji Data.**

Kuna hatari za kutuma data zako kutoka nchi ambako zilikusanywa hadi nchi ambako timu zetu ziko, kama zifuatazo:

- Tukikosa kuambatana na sheria za nchini za faragha ya data, basi inaweza kuwa vigumu kutumia haki zako za faragha katika nchi ambako timu zetu ziko.
- Tukishiriki data zako na wasindikaji wowote wengine nje ya nchi yako, msindikaji huyo huenda asiwe chini ya sheria za faragha ya data za nchi yako. Msindikaji huyo mwingine akiamua kutumia au kushiriki data zako kwa malengo ambayo hayajaelezewa katika Fomu hii ya Idhini ya Data au katika Kauli yetu ya Faragha, inaweza kuwa vigumu au hata isiwezekane kabisa kutumia haki zako za faragha dhidi ya msindikaji huyo mwingine.
- Kuna uwezekano kwamba haki zako chini ya sheria za nchi yako zina kinzana na sheria husika nchini Marekani, na mahakama nchini Marekani zinaweza kufafanua haki zako kwa njia tofauti na mahakama katika Umoja wa Ulaya au nchini mwako.

10. **Hakuna Upatikanaji wa Sheria ya Faragha ya Marekani Kutotosha.**

Tume ya Umoja wa Ulaya iliyo na jukumu la kufanya maamuzi kuhusu utoshelevu wa sheria za faragha za mamlaka nyingine kw kulinganisha na GDPR bado haijapata kwamba ulinzi wa data za kibinafsi nchi ya Marekani unatoa kiwango sawa cha ulinzi kama sheria za faragha katika Umoja wa Ulaya.

Aidha, hatujawasilisha Kauli yetu ya Faragha au yoyote ya sera na taratibu zetu za ndani kwa mamlaka yoyote ya udhibiti ili kubaini kana kwamba zinatimiza viwango vya ulinzi vya GDPR. Kwa hivyo, kuna uwezekano kwamba sera na taratibu zetu hazitoshi chini ya GDPR.

11. **Kuondoa Idhini Yako**

Unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote kwa kuwasiliana nasi kupitia:

**The Worldcoin Request Portal ,**

**548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA**

Ukiondoa idhini yako, basi hatutatumia tena data zako kwa malengo yaliyotajwa hapa juu. Pia unaweza kuamua kufuta data zako kutoka kwenye ndani ya Worldcoin.